MAELEZO MAFUPI YA MKUU WA MKOA WA MOROGORO
MHE. LT.COL.. (MST.) ISSA S. MACHIBYA KWA
RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MHE. DR. JAKAYA MRISHO KIKWETE WAKATI WA ZIARA
YAKE MKOANI MOROGORO TAREHE 29/ - 30/07/2010

- Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete
  Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
- Mhe. Mama Salma Kikwete, Mke wa Rais wetu,
- Mhe. Eng. Petro Kingu - Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Morogoro,
- Mhe. Asha Kipangula - Katibu wa CCM Mkoa – Morogoro,
- Mhe. Chifu Kingalu Mwanabanzi wa 14,
- Ndugu Stephen Bushiri - Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro
- Ndg.Wataalam Mlioongozana na Mheshimiwa Rais
- Wah. Wakuu wa Wilaya
- Wahe.Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa
- Wageni Waalikwa
- Wana Habari,
- Mabibi na Mabwana.

Itifaki imezingatiwa.

1. Awali ya yote, kwa niaba ya Uongozi na wananchi wote wa Mkoa wa Morogoro, na kwa niaba yangu mimi mwenyewe, ninayo furaha kubwa kukukaribisha Mkoani Morogoro wewe Mhe. Rais, pamoja na msafara mzima uliofuatana nao. Tunasema karibuni sana.

2. Mhe. Rais, sisi wananchi wa Mkoa wa Morogoro tunapenda kuungana na Watanzania wenzetu, wapenda Amani na Maendeleo wote nchini kukupongeza wewe binafsi kwa kukubali uteuzi wa Chama cha Mapinduzi kuwa Mgombea wake tena, katika kipindi cha Pili cha Serikali ya Awamu ya nne. Kwa hakika uteuzi wako umeweza kujibu kiu na matarajio makubwa walio nayo Watanzania baada ya kuridhishwa na Utendaji na Utumishi wako mahiri na makini uliouonyesha kwa kipindi cha Miaka 5 ya Serikali ya Awamu ya nne.

3. Kadhalika naomba nitumie hadhara hii kutoa shukrani zetu za dhati kwa Mkutano Mkuu wa CCM ulioketi Mjini Dodoma tarehe 10 – 11/7/2010 kuridhia Mhe. Dr. Mohamed Gharib Bilal kuwa Mgombea mwenza wako kama ulivyowaomba. Tunampongeza sana Mhe. Dr. Mohamed Gharib Bilal kukubali kubeba dhamana hiyo kubwa.

4. Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, kwa niaba ya Wananchi wa Mkoa wa Morogoro tunampongeza sana Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dr. Ali Mohamed Shein kwa kuteuliwa kwake na Halmashauri Kuu ya CCM Taifa kuwa Mgombea wa nafasi ya Urais wa Zanzibar katika Uchaguzi Mkuu ujao mwezi Oktoba, 2010. Kwa pamoja tunawatakia kila la kheri katika kuipeperusha vyema Bendera ya CCM ili hatimaye kupata ushindi wa kishindo.

5. Itakumbukwa kuwa ziara hii ya leo ni ya pili kufanyika katika mkoa wetu kwa mwaka huu wa 2010. Ziara nyingine ni ile uliyoifanya maalum tarehe 06 - 08/02/2010 ulipokuja kuwafariji wahanga wa mafuriko wilayani Kilosa yaliyotokea mwezi Disemba 2009 hadi Januari 2010.

6. Kutokana na moyo huo wa ujasiri uliouonyesha wa kuja kushirikiana nasi katika kuwafariji wahanga wa mafuriko, naomba nichukue fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Morogoro kutoa shukrani zetu za dhati kwako wewe mwenyewe binafsi, kwa Serikali yetu ya Awamu ya Nne na Mashirika mbalimbali ya misaada kwa kuuwezesha mkoa kukabiliana ipasavyo na athari za mafuriko yaliyotokea katika wilaya ya Kilosa.

7. Hali ilivyo sasa ni kwamba idadi ya wahanga waliokuwa wakihifadhiwa kwenye makambi imepungua kutoka kaya 2,010 zenye watu 9,440 hadi kufikia kaya 1,320 zenye watu 5,248.

8. Aidha jumla ya ekari 402 zililimwa na kupandwa mbegu bora za mahindi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu (Kitengo cha Maafa) kwa ajili ya Wahanga, na sasa wanaendelea na uvunaji. Kadhalika mahanga ya mabati 104 yalijengwa kwenye Kambi zote baada ya mahema kudhoofu sana.

9. Hivi sasa tofali 9,680 zimefyatuliwa na kazi hiyo bado inaendelea kwa kasi ya kuridhisha. Pia jumla ya viwanja 931 vimepimwa na kugawiwa kwa wahanga 684 ambapo viwanja 217 vimegawiwa kama fidia kwa watu waliojitolea mashamba yao kwa ajili ya makazi ya kudumu ya wahanga wetu.

Mhe. Rais

10. Nafurahi kukujulisha kwamba zoezi la ujenzi wa Kambi za Wahanga wa mafuriko lilienda sambamba na ujenzi wa visima vya maji ambapo jumla ya visima 9 vifupi vyenye thamani ya Sh.42,000,000/= vilijengwa kupitia ufadhili wa shirika lisilo la Kiserikali la Oxfarm – GB.

11. Kwa ujumla misaada iliyopokelewa toka kwa wahisani mbalimbali ilikuwa yenye thamani ya Sh.5,216,674,060/= kati yake fedha taslimu ilikuwa Sh.1,117,614,510 misaada ya chakula ilikuwa na thamani ya Sh.1,702,554,930, vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh.212,065,000/= vifaa kutoka Serikali ya china Sh.202,650,000/= na vifaa vinginevyo sh.1,982,789,620/=. Napenda kukuhakikishia Mhe. Rais kuwa misaada hiyo yote iligawiwa kwa wahanga kama ilivyokusudiwa, ikijumuisha pia kila mhanga kupatiwa godoro na chandarua kama ulivyoagiza.

Mhe. Rais

12. Baada ya kutoa kwa muhtasari taarifa ya hali ya mafuriko katika wilaya ya Kilosa, sasa naomba nieleza baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hiki cha miaka mitano (2005 – 2010) ambapo Serikali ya awamu ya nne inaelekea kukamilisha awamu ya kwanza ya kipindi chake cha miaka mitano ya awali. Taarifa ya kina ipo katika kitabu cha mkoa chenye taarifa ya shughuli za maendeleo ambacho nitakukabidhi hivi punde.

13. Hata hivyo kabla sijaanza kutoa maelezo hayo ya kisekta, ningependa kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Morogoro kukushukuru sana wewe binafsi Mhe. Rais pamoja na Serikali yetu kwa kutupatia wilaya mpya ya Gairo, ikiwa ni utekelezji wa ahadi yako uliyoitoa wakati wa ziara yako ya tarehe 26 – 29/06/2009 ulipotembelea Jimbo la Gairo na Morogoro Kusini. Tunasema ahsante sana. Baada ya salamu hizo, sasa kwa ridhaa yako naomba nitoe maelezo ya mafanikio ya Kisekta kama ifuatavyo:-

Mhe. Rais

SEKTA YA ELIMU

Elimu ya Awali

14. Kwa upande wa sekta ya elimu, Mkoa umepata mafanikio katika elimu ya awali kwa kuwa na madarasa 623 mwaka 2010 ukilinganisha na madarasa 326 yaliyokuwepo mwaka 2005. Ongezeko hili la madarasa 297 ni sawa na asilimia 47.7. Pia tumeandikisha wanafunzi 34,820 mwaka 2010 ikilinganishwa na wanafunzi 22,971 kwa mwaka 2005. Ongezeko la wanafunzi 11,849 ni sawa 34%.

Elimu ya Msingi

15. Kwa upande wa Shule za Msingi zimeongezeka toka 757 mwaka 2005 hadi 815 mwaka 2010 sawa na ongezeko la asilimia 7.7. Hali kadhalika madarasa yameongezeka toka 2,092 mwaka 2005 hadi 5,143 mwaka 2010 sawa na ongezeko la madarasa 3,051 ikiwa ni 59.3%. Aidha, wanafunzi walioko shule za msingi wameongezeka toka 379,079 mwaka 2005 hadi 414,465 mwaka 2010 sawa na ongezeko la 9.3%.

Mhe. Rais

16. Pia tumefanikiwa kupanda hadi nafasi ya kumi bora kwa ufaulu wa mitihani ya darasa la saba Kitaifa kutoka nafasi ya 20 kati ya mikoa 21 Tanzania Bara mwaka 2005 na kushika nafasi ya 7 mwaka 2007 , na nafasi ya 9 kwa miaka miwili mfululizo (mwaka 2008 na 2009). Vile vile Mdondoko(dropout) umepungua kwa asilimia 50.3 toka wanafunzi 2,022 mwaka 2005 hadi wanafunzi 1,005 mwaka 2010.

17. Idadi ya wanafunzi katika Shule za Msingi nayo imeongezeka toka 379,093 mwaka 2005 hadi kufikia wanafunzi 417,121 mwaka 2010. Ongezeko hili limetokana na mpango wa Maendeleo ya elimu ya Msingi (MMEM). Jumla ya watoto walioandikishwa darasa la kwanza mwaka 2010 ni 50,296.

Mhe. Rais

18. Ongezeko hili la wanafunzi limekuwa likienda sambamba na kiwango cha ufaulu. Takwimu za ufaulu kuanzia mwaka 2006 hadi 2009 ni kama ifuatavyo:

- Mwaka 2006 watoto waliofanya mitihani walikuwa 36,201 kati yao waliofaulu walikuwa 21,715, (59.9%) na waliochaguliwa walikuwa asilimia 84.1.

- Mwaka 2007 waatoto waliofanya mitihani walikuwa 38,228 kati yao waliofaulu walikuwa 21,442 (56.1%) na waliochaguliwa walikuwa asilimia 98.18.

- Mwaka 2009 watoto waliofanya mitihani walikuwa 53,413 kati yao waliofaulu walikuwa 29,995 (56.2%) na waliochaguliwa walikuwa asilimia 96.9.

- Mwaka 2009 watoto waliofanya mitihani walikuwa 53,803 kati yao waliofaulu walikuwa 29,995 (51.7%) na waliochaguliwa walikuwa asilimia 99.9

Mhe. Rais

Elimu ya Sekondari

19. Mkoa unaendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2005) kwa kushirikiana na wananchi kwani tangu mwaka 2005 hadi 2010 jumla ya shule za sekondari 143 zimejengwa kwa ushirikiano wa nguvu za wananchi, Serikali na wadau wengine wa maendeleo.

20. Idadi ya shule za Sekondari zimeongezeka kutoka shule 58 (2005) hadi 199 (2010) kwa mchanganuo wa shule serikali 159 na binafsi 40. Aidha, madarasa yameongezeka kutoka madarasa 418 (2005) hadi 1,281 (2010), wanafunzi wa sekondari waliongezeka kutoka 23,643 (2005) hadi 59,559 (2010) sawa na ongezeko la asilimia 206.5.

Mhe. Rais

SEKTA YA KILIMO

21. Utekelezaji wa shughuli za kilimo msimu wa mwaka 2009/2010

Mkoa wa Morogoro ni kati ya mikoa sita ya uzalishaji ikiwepo Ruvuma, Iringa, Mbeya, Rukwa na Kigoma. Malengo yalikuwa ni kulima hekta 594,952.4 kuvuna tani 2,120,613.7 za mazao ya chakula na hekta 94,339.4 kuvuna tani 1,650,463.3 za mazao ya biashara.

22. Zililimwa hekta 404,403 na kuvuna tani 1,299,694 za Chakula; na hekta 50,307.4 na kuvuna tani 561,651 za mazao ya biashara. Hali ya Chakula ilikuwa ya kuridhisha ingawa kulikuwa maeneo machache yaliyokuwa na upungufu wa Chakula katika wlaya za Kilosa (Tarafa ya Gairo), Mvomero (Tarafa ya Mlali, Kijiji cha Kibati), Morogoro(Tarafa ya Ngerengere, Kijiji cha Mkono wa Mara) na Ulanga (Tarafa ya Mwaya). Mkoa uliwezeshwa kupata msaada wa mbegu bora tani 141(mahindi tani 134, mtama tani 7) yenye kuvumilia ukame toka Ofisi ya Waziri Mkuu, kitengo cha Maafa.

23. Aidha kwa msimu wa mwaka 2009/2010 Mkoa ulipokea jumla ya VOCHA za RUZUKU 358,300 zenye thamani ya sh.6.88 bilioni kwa ajili ya mazao ya chakula (mahindi na mpunga).

Mhe. Rais

25. Kwa upande wa kilimo cha umwagiliaji niseme mazingira yaliyopo yanaruhusu kufanyikaMkoa una mito 143 na mabonde yenye eneo la hekta 425,000 yanayoweza kulimwa kiangazi na pia kutumiwa kwa umwagiliaji. Baadhi ya maeneo ni Bonde la Kilombero na Bonde la Wami . Mkoa una eneo la hekta 123,507 linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji.

26. Hadi sasa ni hekta 17,542.2 na kati ya hizo hekta 8,809 (4%) tu ndiyo zenye miundombinu ya kisasa ya umwagiliaji. Maeneo mengine hutumia mifereji ya asili.

27. Katika kukabiliana na changamoto za upatikanaji wa zana bora za kilimo, Halmashauri zetu zimeweza kuwakopesha wakulima Matrekta madogo (Power Tillers) ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Serikali kwa mchanganuo ufuatao:-

- Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro Vijijini imetoa *Power Tillers* 40, Kilosa imekopesha *Power Tillers* 26, Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga imekopesha *Power Tillers* 12, Mvomero *Power Tillers* 10, Morogoro Manispaa imekopesha *Power Tillers* 3. Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero inatarajia kupokea *Power Tillers* 23 ifikapo tarehe 11/08/2010 na kuzikopesha kwa wakulima wake. Wilaya hii imechelewa kupata matrekta haya kwa sababu Mzabuni aliyepewa Kandarasi ya awali kujitoa dakika za mwisho na kuilazimu Halmashauri kutangaza zabuni hiyo upya.

- Pia Mkoa ulipata msaada wa Trekta moja aina ya *Massey Ferguson* kutoka Kampuni ya *Tractors Limited,* Tawi la

Morogoro ambalo tumelikabidhi kwa Halmashauri ya Wilaya Kilosa kusaidia wakulima.

Mhe. Rais

Sekta ya Afya

27. Kwa upande wa sekta ya Afya mkoa umejipanga vyema katika kukabiliana na maambukizi mapya ya ugonjwa wa UKIMWI ambapo kwa sasa maambukizi ni asilimia 5.2. Aidha katika kutekeleza Mpango wa MMAM kupitia Ilani ya uchaguzi kwa kuhakikisha kuwa kila kijiji kinakuwa na zahanati yake,Mkoa umejipanga vilivyo katika kufikia malengo hayo ambapo kila kijiji hulazimika kufyatua tofari zake na kuchangia nguvu kazi.Mpaka sasa mkoa una Zahanati 183 kati ya mahitaji ya zahanati 593 na vituo vya afya vilivyopo ni 27 kati ya mahitaji ya vituo 181.

Mhe. Rais

Sekta ya Barabara

28. Kuhusu sekta ya barabara, mkoa unatoa shukrani zake za dhati kwa serikali ya Awamu ya Nne kwa kutimiza ahadi yake ya kuanza kutekelezwa miradi mikubwa miwili iliyoahidiwa katika Ilani ya

Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 – 2010. Miradi hiyo ni ile ya ujenzi wa daraja la mto Kilombero na barabara ya Mikumi – Kilosa – Dumila – Turiani – Mziha - Handeni. Hatua iliyofikiwa katika miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

- **Ujenzi wa Barabara ya Dumila – Rudewa (Km. 45)**
  Usanifu wa kina wa barabara umekamilika na ujenzi wa sehemu hii umeanza na unafanywa na Mkandarasi M/S China Civil Engineering Construction Corporation mbapo kazi imeanza tareh 1/2/2010 kwa gharama ya shs.41,929,601,023.17. Ujenzi huu ambao ni wa kiwango cha lami utachukua muda wa miezi 24 hadi utakapokamilika.

- **Mziha - Turiani - (km 36) - Magole (km 48.6)**
  Ujenzi wa sehemu ya Turiani – Magole umeanza na unafanywa pia na Mkandarasi M/S China Civil Engineering Construction Corporation ambapo kazi imeanza mwezi Machi 2010 kwa gharama ya shs. Bilioni 42.

  Ujenzi huu ambao ni wa kiwango cha lami utachukua muda wa miezi 30 hadi utakapokamilika. Aidha kwa upande wa barabara ya Turiani - Mziha (Km 36) usanifu wa kina (Detailed Engineering Design) umekamilika na umefanywa na kampuni

ya kihandisi ya KAPSEL kutoka Dar es Salaam.Ujenzi kamili utaanza baada ya fedha za ujenzi kupatikana.

- **Ujenzi wa Daraja la Mto Kilombero**. Usanifu wa kina (Detailed Engineering Design) umekamilika na ujenzi utaanza mwaka huu wa fedha wa 2010/2011 ambapo serikali imetenga kiasi cha sh.3.5 bilioni kwa ajili ya kazi hiyo.

- **Ujenzi wa barabara ya Ifakara - Kihansi**
  Katika kutambua umuhimu wa bonde la Kihansi katika utekelezaji wa agizo la Kilimo Kwanza, serikali imetenga kiasi cha sh.milioni 287.2 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu (Feasibility Study) na usanifu wa kina (Detailed Engineering Design) ni matumaini ya mkoa kuwa endapo barabara hii itaimarishwa basi malengo ya kufikia Mapinduzi ya Kijani yatafikiwa.

Mhe. Rais

29.Suala lingine ambalo ningependa kutoa taarifa kwako ni kuhusu utekelezaji wa agizo lako la kukamilisha ujenzi wa Daraja la mto

Mtombozi na daraja la Magogoni katika wilaya ya Morogoro.Madaraja hayo yote yamekamilika na yanatumika kwa sasa.Muhtasari wa gharama ni kama ifuatavyo:-

- **Daraja la Mtombozi**

  Daraja hili limegharimu kiasi cha sh.310,115,000 na kipande cha barabara cha km 10 kilichofunguliwa kimegharimu kiasi cha sh.99,800,000.Ujenzi wa daraja hili umesaidia kufungua soko kwa mazao ya wakulima katika eneo hilo na vijiji jirani.

- **Daraja la Magogoni katika mto Ruvu.**

  Daraja hili lenye urefu wa mita 57.92 na uwezo wa kupitisha magari yenye uzito wa tani 36 limegharimu kiasi cha sh. 128,430,000.Kukamilika kwa daraja hili kumeimarisha usafirishaji wa mazao ya chakula na biashara kutoka vijiji vya Kisaki,Duthumi,Mvuha na maeneo jirani kwenda Dar es salaam bila kupitia Morogoro Mjini.

Mhe. Rais

30. Nisingependa kukuchosha na maelezo mengi. Haya ni baadhi tu ya mafanikio yaliyopatikana kwa baadhi ya sekta katika mkoa wetu wa Morogoro katika kipindi hiki cha serikali ya awamu ya Nne.Maelezo ya sekta zote yapo katika kitabu chenye maelezo ya Mkoa.

31. Mwisho, Mhe.Rais nikuhakikishie kwamba Serikali ya Mkoa wa Morogoro kwa ushirikiano na Halmashauri za Wilaya/Manispaa wananchi, Wadau , Wahisani na Asasi mbalimbali wote kwa pamoja wamepanga kutekeleza majukumu yao kikamilifu katika kujiletea Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii. Mafanikio yaliyopatikana katika Serikali ya Awamu ya IV (2005-2010) ni Matokeo ya Uongozi wa pamoja ya uwajibikaji na uwazi katika kuleta maendeleo stahimili (Sustainable Development).

32. Aidha Mkoa wa Morogoro unatarajia kulinda, kudumisha, kuboresha na kuendeleza mafanikio yote yaliyopatikana katika Serikali ya Awamu ya Nne. Kwa kutumia falsafa ya Ari Zaidi, Nguvu Zaidi na Kasi Zaidi na tutaendelea kwa juhudi zote kuleta maendeleo endelevu kwa wananchi wote Mkoani Morogoro.

Mhe. Rais,

Mwisho naomba nikushukuru kwa kunisikiliza.

Naomba kuwasilisha.

Issa Salehe Machibya,
Luteni Kanali (Mstaafu)
MKUU WA MKOA